

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Nne – Tarehe 4 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Tukae, Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na swali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe, kwa niaba.

Na. 26

Kuwasaidia Watoto Wenye Ulemavu

MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. ALI HASSAN OMAR KING aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawatambua watoto wenye ulemavu ambao wanaishi kwenye mazingira magumu ili kuwasaidia kwa matibabu na kimaisha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA,
VIJANA NA WENYE ULEMAVU) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwatambua na kuwapatia huduma stahiki watu wenyewe ulemavu ikiwa ni pamoja na waishio katika mazingira hatarishi zaidi kwa kuzingatia aina ya ulemavu walionao na hitaji la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi huo umekuwa ukifanyika kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenyewe Ulemavu ya mwaka 2004. Kwa kuzingatia sera hiyo, Serikali imemeanzisha Rejesta ya Utambuzi wa Watoto Waishio katika Mazingira Hatarishi zaidi. Serikali imeweka pia mfumo wa ulinzi na usalama wa watoto. Aidha, Serikali imekamilisha Mwongozo wa Utambuzi wa Mapema wa Afua na Stahiki za Watoto wenyewe Ulemavu wa mwaka 2021 unaoainisha namna sahihi ya kumtambua mtoto mwenye ulemavu na afua anazostahili kupatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wenyewe ulemavu waishio katika mazingira hatarishi zaidi hupatiwa huduma kupitia afua mbalimbali ikiwemo kupatiwa elimu kupitia shule zenye vitengo maalum na jumuishi; kuwapeleka katika hospitali kwa ajili ya kupatiwa afua za matibabu, kupatiwa stadi za maisha kwa lengo la kuwajengea uwezo ili wawzeze kujitegemea na kujilinda; kupatiwa uchangamshi wa awali na huduma za utengamao; kuwarejesha katika familia zao na kuwaweka katika familia za kuaminika (*fit family*); utoaji wa vifaa saidizi; kuwaunganisha na vyuo maalum vya watu wenyewe ulemavu kwa ajili ya kupatiwa ujuzi na huduma za marekebisho na kwa wale ambao hawana walezi au wazazi hupelekwa kwenye makao ya watoto kwa ajili ya huduma mbalimbali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ali King.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri maana yamekuwa safi tofauti na *penalty* ya Simba ya jana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba hawa watoto wenyewe walemauvu mara nyingi huwa wanarandishwa randishwa mitaani na unaweza ukaja ukamkuta mtoto anarandishwa mtaani na watoto wenziwe maana yake mpaka hawa wengine wanakosa zile haki za watoto.

Sasa ndio maana nikauliza ni lini kwa sababu tunaona bado wako mtaani wanarandishwa ni lini hasa hatua stahiki za ukweli ukweli zitachukuliwa ili kupunguza lini wimbi? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalii la pili wazee wengi huwa wanashindwa hizo huduma tunazoambiwa wanapewa wanashindwa kuwapelekwa watoto hawa kwenda kupata huduma, wengine wanahitaji kwenda kupelekwa kwenye mashine kufanyishwa mazoezi, lakini wengine wanahitaji mambo tofauti tofauti, lakini ingawa limejibowiha hapa lakini tunaona kwamba ni bado hicho kitu kinaendelea.

Kwa hiyo niiulize Serikali ni lini hili jambo la watoto kupatiwa hizi huduma ambazo wanahitaji wakati mwininge zinatolewa kwa pesa watapata bure ili wale wazee nao waweze kupata faraja? Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali King, la kwanza akiuliza kwamba hawa watoto wamekuwa wakirandishwa randishwa mitaani kwa maana ya kuzururishwa.

Ni lini hatua stahiki zitachukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali wamekwisha kuanza kuchukua hatua hasa pale matendo kama hayo yanapofanya mitaani na kwa kuzingatia mwongozo huo ambaao umetolewa ambaao ni Mwongozo wa Taifa Utambuzi wa Mapema Afua Stahiki za Watoto wa Watu Wenye Ulemau. Lakini pia kwa mujibu wa sheria tulizonazo na moja ya sheria ni hizo za utekelezaji wa sheria za watoto ambapo watoto wana haki na stahili zao zimeainishwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa hiyo, pale inapobainika kwamba kuna changamoto kama hizo kwenye mitaa yetu hatua zimekuwa zikichukuliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa sababu zimeainishwa kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2019. Kwa hiyo, hatua tayari tumekwisha kuanza kuchukua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri inatosha ameshakuelewa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu huduma; tayari Serikali imekwisha kutambua watoto zaidi ya 76,247 na ilibaini watoto wenye changamoto hizo ni 42,373 na hivyo tayari umekwisha kuingia kwenye mpango kupitia rejista ambayo iko ya utambuzi chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, lakini sambamba na hilo pia Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea na shughuli hiyo ya usimamizi na uratibu wa masuala ya ulinzi na usalama wa Watoto, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Zaytun una swali?

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo.

Na.27

Kuwatafutia Vijana Ajira na Fursa Nje ya Nchi

MHE. ALI JUMA MOHAMED aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia ajira na fursa mbalimbali nje ya nchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mpango mikakati ifuatayo ili kuunganisha vijana na fursa za ajira nje ya nchi:-

(i) Imeingia makubaliano (*bilateral agreements*) na baadhi ya nchi zenye fursa za ajira duniani.

(ii) Imeweka mwongozo wa kuratibu shughuli za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira ili kuwezesha shughuli za kuunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi kufanyika kwa kuzingatia haki za msingi za wafanyakazi na viwango vya kazi vinavyokubalika na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Hadi sasa jumla ya Wakala 58 wamesajiliwa na kupewa leseni, kati ya hao Wakala watano wanajishughulisha na kuwaungaunisha watafuta ajira nje ya nchi.

(iii) Kujenga mfumo wa kielektroniki wa huduma za ajira utakaorahisisha na kuweka uwazi katika kuratibu upatikanaji wa fursa za ajira nje ya nchi; mchakato wa kuandaa Watanzania wenye sifa pamoja na kufuatilia hali za Watanzania wakiwa wanafanya kazi nje ya nchi. Mfumo unatarajiwa pia kukamilika na kuanza kutumika kabla ya mwezi Juni, 2022.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu katika mpango huo ni kutekeleza Programu ya Taifa ya Mafunzo ya Ujuzi hususani kuitia mafunzo ya uanagezi pamoja na utarajali ili kuwezesha vijana husika kuwa na ujuzi stahiki kufanya kazi nje ya nchi.

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tano baadhi ya machache hayo nikiyataja kwa sababu ya muda kufanya marekebisho Sheria ya Huduma za Ajira ya mwaka 1999 pamoja na Kanuni za mwaka 2014 ili ziweze kuendana na mazingira ya sasa ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ali.

MHE. ALI JUMA MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani kwa kutumia ofisi zetu za kibalozi kuwasaidia wale vijana wetu wa Kitanzania ambao tayari wameshapata fursa ya kufanyakazi nje ya nchi, lakini mara kwa mara wamekuwa wakipata matatizo na shida ambazo wanakosa kusaidiwa?

Lakini la pili Serikali ina takwimu rasmi za vijana wote ambao wanafanyakazi nje ya nchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu, swali fupi; jibu fupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mohamed kwa kuangalia sana haya maslahi ya ajira ya Watanzania nimpongeze sana kwa kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu, Ofisi ya Waziri Mkuu inashirikiana vizuri na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kwa kuhakikisha kwamba masuala haya yanaratibiwa vizuri na

hata hivi sasa tumekwisha kuanza utambuzi huo wa vijana wapo ambao walikuwa wanaenda wenyewe bila kutoa taarifa kwenye ubalozi au kwenye nchi na wamekuwa wakipata matatizo mbalimbali tumewaomba na tumetoa rai kwamba waendelee kujisajili kwenye Balozi zetu.

Lakini zaidi ya hapo pia katika mikataba ambayo tumeingia sasa maalum, kwa mfano Qatar tunakuwa na Kombe la Dunia hivi karibuni wafanyakazi wengi tunatarajia kuwapeleka kule na waweze kupata ajira.

Kwa hiyo, haya tunayaratibu vizuri kupitia Wizara ya Mambo ya Nje kwa kushirikiana na balozi zetu huko nchini na hivi karibuni mmeona Balozi wa Ubelgiji alitoa takwimu za maeneo ambayo Watanzania wangeweza kuchangamkia kuweza kupata ajira. Kwa hiyo uratibu upo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu katika maeneo hayo.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu mazuri. Tunaendelea Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Elbariki Kingu.

Na 28

Ujenzi wa Zahanati-Singida Magharibi

MHE. FLORENT L. KYOMBO K.n.y. MHE. ELIBARIKI I. KINGU
aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza maboma ya Zahanati ya Ufana, Kinyampembe, Mpeti, Misake, Mlandala, Kaugeri na Mtavira ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi kwa zaidi ya miaka mitano sasa katika Jimbo la Singida Magharibi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kujenga vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha utoaji wa huduma za afya ya msingi kwa wananchi ikiwemo ukamilishaji wa maboma ya zahanati. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 28.2 za ruzuku kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 564 katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Disemba, 2021 tayari Serikali imepeleka shilingi bilioni 15.4 katika Halmashauri nchini kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti iliyopangwa ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 200 kimepelekwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kutekeleza ukamilishaji wa maboma ya zahanati nne za Ufana, Kinyampembe, Misule na Makotea. Aidha, Halmashauri kutumia mapato ya ndani imetenga shilingi milioni 50 kukamilisha boma la zahanati ya Kaugeri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka mpango wa kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, Serikali inazielekeza Halmashauri zote nchini kuendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hizo ili ziweze kutoa huduma tarajwa kwa wananchi, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kingu.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zimekuwa zikitolewa na Serikali kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa maboma fedha nyingi zimeonekana zimeshindwa kuyakamilisha

maboma yaani kiwango cha shilingi milioni 50 zinakwenda kwenye vijiji lakini maboma hayaishi.

Je, Serikali imefanya tathmini ya kina kujua kwamba /leve/ya maboma iliyofikiwa kwa nguvu za wananchi inahitaji fedha kiasi gani ili kumaliza maboma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ninaomba kumuuliza Waziri ni lini sasa Serikali itapeleka watumishi katika zahanati ambazo zimetengewa fedha na kukamilika ili kuhakikisha wananchi wetu wote wanapata huduma katika zahanati husika katika maeneo husika? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Kingu kwa uchapakazi wake mzuri kwa kuwasemea wananchi wa Jimbo la Singida Magharibi na kwa kweli Serikali tutaendelea kumpa ushirikiano kuhakikisha wananchi wanapata miradi hiyo ya maendeleo kwa ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ambazo zimepelekwa kwenye ukamilishaji wa maboma ya zahanati, kila boma ambalo limefikia hatua ya lenta linatengewa shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji na tathmini ilifanyika kwa sababu ramani zile zilitolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na BOQ zake zilionesha jengo likijengwa mpaka hatua ya lenta likipewa shilingi milioni 50 jengo lile linakamilishwa bila changamoto yoyote na ndiyo maana katika maboma 555 yaliyopelekewa takribani shilingi 27,750,000,000 mwaka wa fedha uliopita zaidi ya asilimia 85 ya maboma yamekamilika, yameanza kusajiliwa kwa ajili ya kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tathmini ilifanyika, lakini kuna *variation* za kimazingira za hapa na pale ambazo nazo huwa tunazizingatia na kama inajitokeza *variation* kama hiyo basi tunaona namna nzuri ya kukamilisha ujenzi wa zahanati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili ujenzi wa zahanati na vituo vyaa afya kwa ujumla wake unakwenda sambamba na mpango mkakati wa kuajiri watumishi ili zahanati na vituo vianze kutoa huduma na tayari Serikali tumefanya tathmini ifikapo Juni, 2022 tutakuwa na vituo 1,073 ambavyo vitakuwa vimekamlika na tumeshafanya tathmini ya mahitaji ya vifaa tiba, lakini pia na watumishi na kwa kadri ya bajeti yetu tutaendelea kupeleka watumishi ili vituo vile vianze kutoa huduma na kupunguza upungufu wa watumishi katika maeneo hayo, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tarime inaelemewa kwa kupokea wagonjwa wengi kutoka nje ya mji wa Tarime mathalani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Serengeti, Ranya na hata wakati mwingine kutoka nchi jirani ya Kenya.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kukamilisha kituo cha afya cha Kenyamanyori pamoja na zahanati ya Nyandoto ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi ili walau kupunguza *pressure* ambayo inapelekea msongamano katika hospitali ya Mji wa Tarime?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuhakikisha tunajenga zahanati na vituo vya afya ili kupunguza kwanza umbali wa wananchi kupata huduma, lakini pili kupunguza msongamano kwenye hospitali za Wilaya kama ilivyo katika hospitali ya Wilaya ya Tarime.

Kwa hivyo suala hilo ni la msingi na mipango hiyo tayari imewekwa, wito ambao nautoa kwa Halmashauri ya Tarime ni kutoa kufanya tathmini ya mahitaji ya fedha zinazotakiwa kukamilisha kituo cha afya na zahanati, pili kutenga kuititia mapato ya ndani, lakini pia Serikali Kuu tunaendelea kuangalia fursa ya kupeleka fedha ili kukamilisha zahanati hizo, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Vita halafu Mheshimiwa kutoka Mwenyekiti wa Bajeti.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona changamoto ya Jimbo la Singida ziko sambamba kabisa na changamoto ambazo zinaikabili wilaya ya Chunya kwenye umalizajji wa maboma; kuna boma liliojengwa kwa nguvu ya wananchi kwenye kata ya Ifumbo lina zaidi takribani miaka minne halijakamilika.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili ukamilishaji wa boma hili kwenye kata ya Ifumbo iweze kukamilika ilihali ukijua kata hii iko mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ni lini, jibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu la Mheshimiwa Kasaka, Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati tumeainisha maeneo ya kimkakati, na tuliwaomba Waheshimiwa Wabunge kuwasilisha vipaumbele. Ni muombe Mheshimiwa Mbunge, kama Kituo cha Afya katika Kata ya Ifuko ni kipaumbele basi tupate

taarifa hiyo rasmi ili tuweze kuweka mpango wa kuhakikisha kwamba tunakamilisha ili wananchi wapate huduma. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kawawa, ajiandae Mwenyekiti wa Bajeti.

MHE VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Je, Serikali inaweza kutuweka katika orodha vijiji vyetu vya Ulamboni, Kilangalanga, Chengena, Luhangano na Mhangazi vyenye maboma ambayo hayajaisha ili waweze kupata hizo shilingi milioni 50 waweze kumalizia?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa maboma ya zahanati na vituo vya afya kote nchini unafanywa kwa fedha za Serikali Kuu pamoja na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri. Kwa hiyo, kuna vile vituo ambavyo vitakamilishwa kwa fedha za Serikali Kuu na hivyo tumeviainisha, lakini ukitokea uhitaji tutaainisha pia vikiwemo hivi vituo vya Kilangalanga na vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitoe wito kwamba ujenzi wa zahanati hizi ni lazima pia Halmashauri kupiti mapato yake ya ndani, kupitia asilimia 40 ya fedha za miradi ya maendeleo au asilimia 60 watenge fedha kwa ajili ya kukamilisha baadhi ya maboma, wakati Serikali Kuu pia inatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Kawawa kwamba tumelichukua hilo na tutawasiliana kuona yapi yakamilishwe kwa mapato ya ndani na yapi tutafute fedha kutoka Serikali Kuu.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Mwenyekiti, wa Bajati halafu Mheshimiwa Cosato Chumi na kisha Mheshimiwa Pallangyo.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo kwa Mheshimiwa Waziri.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumailizia Kituo cha Afya cha Gidas ambacho kinahudumia si tu wananchi wa Kata ya Gidas ila pamoja na wananchi wa mipakani mwa Kondoa? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati njema wiki iliyopita tulikuwa kwenye ziara jimboni kwake na tulipita katika maeneo haya ikiwepo katika Kituo cha Afya cha Gidas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie, kama tuliviyokubaliana kwamba kituo kile ni cha kimkakati, tutakwenda kutafuta fedha ili kukikamilisha ili tuweze kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chumi halafu Mheshimiwa Pallangyo.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mji wa Mafinga nadhani ndiyo hospitali inayohudumia Halmashauri nyingi kuliko hospitali yoyote hapa nchini. Hospitali ya Mji wa Mafinga inahudumia zaidi ya Halmashauri tano ikiwepo ya Mlimba ambayo iko Mkoa wa Morogoro. Sasa kutokana na unyeti huo, na kwamba iko kando ya barabara kuu.

Je, Seikali iko tayari kuleta watumishi katika mpango wa dharura?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Mafinga ni kweli iko barabarani na inahudumia wananchi wengi; na hospitali zote ambazo ziko kimkakati tunazia inisha na kuziwekea mpango, kwanza wa kupeleka vifaa tiba, lakini pia kuboresha upatikanaji wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie kwamba tutakwenda kwa utaratibu wa kawaida wa kupata watumishi kwa ajili ya hospitali ile badala ya utaratibu wa dharura, kwa sababu utaratibu wa watumishi unapatikana kupitia vibali maalum; laini tutaaipa kipaumbele Hospitali ya Mji wa Mafinga.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pallangyo. Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda majibu mazuri ya Serikali ndiyo hayo, pesa zipo na vituo vyote vitamalizwa. Mheshimiwa Pallangyo. (*Makofi*)

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunionna.

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, je ni lini Serikali itaunga mkono juhudzi za wananchi katika ujenzi wa zahanati za Nsengoni, Gaisosya, Kikatiti na Samaria? Wananchi wamehanganya kuzijenga zahanati hizi kwa miaka minge lakini hawaoni *support* ya Serikali.

MWENYEKITI: *Support*ipo sasa, hela zipo. Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu kweli swali la msingi, mwaka wa fedha uliopita zaidi ya shilingi 27,750,000,000 zilipelekwa ili kukamilisha maboba 555, lakini katika mwaka wa fedha huu wa 2021/2022 zaidi ya shilingi bilioni 28.2 pia zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha maboma 564 ya zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba...

MWENYEKITI: Ahsante, pelekeni pesa. Tunaendelea, Mheshimiwa Salma Rashid Kiwete, kwa niaba.

Na. 29

Hitaji la Kivuko – Mchinga

MHE. ERIC J. SHIGONGO K.n.y. MHE. SALMA R. KIKWETE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kivuko kutoka Mchinga Moja kwenda Mchinga Mbili ili kurahisisha huduma kwa wananchi ikiwemo wanafunzi wanaovuka bahari kwa miguu kwenda Shule ya Sekondari Mchinga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Mchinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa changamoto ya kivuko katika barabara ya Mchinga – Kijiweni, eneo la kutoka Mchinga Moja kwenda Mchinga Mbili lililo katika Jimbo la Mchinga, Wilaya ya Lindi. Serikali kupitia *TARURA* Mkoa wa Lindi, imeshafanya tathimini ya awali ya kutatua changamoto hiyo ambapo kiasi cha shilingi milioni 147 kitaweza kujenga kivuko cha waenda kwa miguu (*pedestrian suspended bridge*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 *TARURA* Wilaya ya Lindi itatenga bajeti ya kiasi cha shilingi milioni 147 kwa ajili ya kujenga kivuko cha waenda kwa miguu. Aidha, ujenzi wa kivuko hicho utaondoa changamoto ya usafiri na usafirishajji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara katika Jimbo la Mchinga kulinga na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shigongo.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Kwa sababu mahitaji ya wananchi wa Mchinga ni kufanya biashara na kuongeza kipato, na kivuko hiki ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa jimbo hili. Ningependa kupata tamko rasi la Serikali kwamba ni lini hasa watarajie kwamba ahadi hii ya Serikali itatekelezwa? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kujibu swali dogo la nyongeza Mheshimiwa Shigongo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali la msingi, Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua ni lini hasa. Nimemueleza hapa kwamba tulishafanya tathmini, na daraja hilo linahitaji shilingi milioni 147, na imetengwa katika bajeti ambayo tutapitisha katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika mwaka wa fedha unaokuja daraja hili litajengwa, na hiyo nina uhakika kwa asilimia 100. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Aida!

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo Mchingga zinafanana sana na Changamoto za Wilaya ya Nkasi katika Kata ya Isunta na Kata ya Namanyele ambako kivuko hicho kimekuwa kikiathiri sana wanafunzi wanaokwenda *Mkangale primary* pamoja na sekondari ya Mkangale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itajenga kivuko hiki ili kuwasaidia watoto ambao wamekuwa wakipata shida sana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu, ni lini? Kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, kama nilivyoeleza awali, madaraja yote yakiwemo yaliyo katika jimbo lake tumeshayafanya tathmini, na mengi tunatarajia kuyaweka katika bajeti hii inayokuja ya mwaka 2022/2023. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatekeleza ahadi hii ambayo Serikali imeahidi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea.

Na. 30

Kutoa Elimu ya Utunzaji Mazingira kwa Wananchi

MHE. BONNAH L. KAMOLI aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kutoa elimu ya utunzaji mazingira kwa wakulima wa mbogamboga ikiwemo pamoja na hatua za kuchukua ili kulinda mazingira katika Bonde la Mto Msimbazi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imebaini uharibifu wa mazingira ya Mto Msimbazi unaofanya na wananchi wanapofanya shughuli si za kilimo tu bali pia uchimbaji wa mchanga pamoja na umwagaji maji machafu kwenye Bonde la Mto Msimbazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, katika kuhakikisha kwamba wakulima wa mbogamboga pamoja na wadau wengine hawaharibu mazingira ya Mto Msimbazi, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa programu maalum za kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya matumizi ya mwongozo wa mita 60 kwa lengo la kunusuru mazingira ya vyanzo vya maji ikiwemo Mto Msimbazi.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rasi kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*)imeelimisha watendaji wa Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kuhamasisha wananchi wanaofanya shughuli za kimaendeleo kwenye Bonde la Mto Msimbazi kuzingatia kanuni na miongozo ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia mabalozi wa mazingira imeanza utekelezaji wa kampeni kabambe ya hifadhi na usafi wa mazingira ambapo suala la hifadhi ya vyanzo vya maji ni moja ya eneo la kipaumbele katika utekelezaji wa kampeni hiyo. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bonnah.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza tunaunga mkono jitihada za Serikali. Hata hivyo, kuna wananchi ambao wanafanya shughuli zao za kilimo cha mbogamboga ambazo zinawaingizia kipato, wako ndani ya mita 60; na shughuli zao hizo haziathiri mazingira.

Je, Serikali iko tayari kuwasaidia wananchi hao au kuwalinda ili wazidi kujiongezea kipato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa eneo hili linaweza likageuzwa kuwa vivutio au sehemu ambazo ni *center* ambazo wananchi wanawenza wakatengeneza, kama vile *Coco Beach* au sehemu nyingine, wakawenza kupata shughuli za kuijendeshea maisha yao.

Je, Serikali iko tayari kuwasiliana na Halmashauri zetu ili wananchi wetu ambao wanaweza kufanya shughuli hizi waweweza kupewa maeneo haya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Segerea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la mita 60 ni jambo la kikanuni kabisa. Lakini kingine tunaweza tukawaruhusu wakaendelea ndani ya mita 60; lakini changamoto iliyopo, athari za kimazingira si athari za kuonekana leo na kesho. Huwezi ukachimba mgodi leo, ukawa unachimba dhahabu au chochote ukaziona athari leo. Huwezi kukata miti ukaona athari leo, huwezi ukaendesha viwanda ukaona athari leo. Kwa hiyo ni jambo ambalo ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo na kesho inawezekana wananchi wa Segerea wanaweza wasione athari za kimazingira, lakini baada ya muda watakuja kuona athari za kimazingira. Hicho ndicho kitu ambacho sisi Serikali tunakihofia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni vipi tutawasaidia, tuko tayari kuwasaidia kwa kuendelea kuwapa taaluma ili sasa waweze kufahamu mambo haya ili wajue athari za kimazingira. Kwa sababu tusipoyalinda mazingira hayataweza kutulinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lingine kwamba je, Serikali iko tayari kuwatengenezea *creation centers* kwa ajli ya angala ya kuweza kuijendesha. Hilo jambo wala hatuna tatizo nalo kwa sababu lengo letu ni kwasaidia wananchi; lakini nadhani watupe muda kwanza ili tutafute fedha kwa sababu hili jambo linahitaji fedha. Kupageuza pale ili tutengeneze sehemu ya kivutio yenye *garden* nzuri tunahitaji tupate fedha za kutosha. Lakini pia watupe muda ili tuweze

kufanya ushauriano na baadhi ya wadau wengine maana pale Wizara za Maji, Maliasili na Ardhi, pamoja na sisi na Halmashauri zinahusika. Kwa hiyo jambo hilo linawezekana, lakini watupe muda kidogo ili tujue namna ambavyo tunafanya. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Neema.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru; kwa kuwa leo ni Siku ya Saratani Duniani, ningependa kuiuliza Serikali, ina mkakati gani wa kuzuia wenyewe viwanda ambao wanachepusha machi yenye kemikali ambazo si salama? Maji haya yanakwenda kwenye Mto Msimbazi na ndiyo maji hayo hayo ambayo hawa wakulima wa mbogamboga wanatumia katika kuzalisha na kumwagilia mbogamboga hizi, hivyo kuhatarisha usalama wa chakula (*food safety*) na hatimaye usalama wa hali ya afya ya wananchi na hivyo uwezekano wa kuchangia katika saratani ni mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kujibu swali la Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumebaini kuwa kuna baadhi ya shughuli nyingine za kibinadamu zinasababisha uchafuzi wa mazingira, zikiwemo hizo ambazo amezitaja, za viwanda na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali kuititia Ofisi ya Makamu Rais, Muungano na Mazingira tunazo jitihada Madhubuti ambazo huwa tunazichukua katika kuhakikisha kwamba tunazuia mambo haya ili kuweza kuzuia athari kwa wananchi, ikiwemo hiyo milipuko ya maradhi, yakiwemo ya kansa na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tunaendelea kutoa taaluma kwa hawa wanaofanya shughuli hizi za kibinadamu, lakini la pili kuna wakati tunatoa hata faini ili waweze kuacha na iwe funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile huwa tunafanya *operations* za mara kwa mara kwenye haya maeneo ya uzalishaji, lengo na madhumuni ni kwamba wanaozalisha wajue kwamba wanazalisha lakini wananchi nao wanaathirika. Lakini zaidi tunafika hatua mpaka tunazuia. Inafika wakati kuna kiwanda kinafanya visivyo, kuna *shell* inafanya isivyo, kuna migodi inafanya visivyo. Kisheria, kwa mujibu wa utaratibu tunazuia uzalishaji ili sasa shughuli nyingine au taratibu nyingine za uhifadhi wa mazingira ziweze kuendelea. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asya.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na ukosefu wa taaluma za kimazingira katika Bonde la Mto Msimbazi ambayo husababisha uchafuzi wa kimazingira kutokea, hali kadhalika ukosefu huu wa elimu unawahusu hasa wavuvi ambapo bahari yetu imechafuka sana na tunakosa samaki wenye afya kutohana na wavuvi kwenda na *plastics* na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusikia Serikali ina mkakati gani, kwanza kuismamia rasilimali hii muhimu ya bahari, lakini la pili, kutoa taaluma kwa wavuvi wetu ili rasilimali yetu iwe salama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kujibu swali lingine la Mheshimiwa Asya, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi kubwa tunayofanya kama Serikali na kama Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ni kuwapa wananchi elimu; na ni kwa sababu tumeefika wakati tumegundua kwamba elimu pekee ndiyo itakayotuokoa sisi kutokana na mazingira machafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wavuvi tumefanya jitihada kubwa. Kaskazini Uguja, kwa sababu kuna bahari tumewapa elimu, Kaskazini Pemba, Kusini Pemba na maeneo yote ya Tanzania yenye visiwa, mito, maziwa pamoja na bahari ambamo shughuli za uvuvi zinafanyika tumejitahidi sana tumewapa taaluma na taaluma inafanya kazi, na tutandelea kufanya hivyo. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Selemani Kakoso.

Na. 31

**Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Tanganyika Kwenda Makao
Makuu ya Mji wa Mpanda**

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya mradi mkubwa wa maji toka Ziwa Tanganyika kwenda Mpanda Mjini ili kutatua tatizo la maji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijiji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa huduma ya maji katika mji wa Mpanda ni wastani wa asilimia 60. Katika kuboresha huduma ya maji katika mji huo, Serikali mwishoni

mwa mwezi Februari, 2022 itaanza utekelezaji wa miradi ya Kanoge II na Shangala. Kazi zitakazoteklezwa ni ujenzi vidakio vya maji vitatu, kufunga pampu, kujenga nyumba ya mitambo (*pump house*), ujenzi wa tenki lenye ukubwa wa mita za ujazo 200 na mtandao wa kusafirisha maji umbali wa kilometra 28. Miradi hiyo ipo kwenye hatua za manunuzi na inatarajiwa kutekelezwa kwa muda miezi sita na kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 6,000 hadi kufikia 8,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mrefu, Serikali imefanya tathmini ya awali ya kutumia Ziwa Tanganyika kuwa chanzo kuu cha maji kwa Mji wa Mpanda na maeneo ya kandokando mwa ziwa hilo. Katika mwaka 2021/2022 Wizara itakamilisha usanifu wa miundombinu inayohitajika kwa ajili ya utekelezaji mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mji wa Mpanda ni mionganini mwa miji itakayonufaika na mradi wa miji 28 na wakandarasi wataanza kazi katika mwaka wa fedha 2021/2022. Miradi hiyo itasaidia kufikia malengo ya kisekta yaliyopo ya zaidi ya asilimia 85 vijijini na zaidi ya asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2025.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali, lakini niishukuru sana Wizara ya Maji kuititia kwa Waziri mwenye dhamana wamefanya kazi kubwa sana ya kipeleka huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa ya Mkoa wa Katavi tunahitaji kupata chanzo cha uhakika cha maji na chanzo hicho kipo Ziwa Tanganyika ambalo linaweza likatatua tatizo la maji kwa kipeleka huduma kwa Wilaya zote tatu kwa maana ya Wilaya Tanganyika, Wilaya ya Mlele na Wilaya ya Mpanda.

Ni lini Serikali itakuja kutatua tatizo la kupeleka huduma ya maji kuliko kutumia fedha nyngi wanazotumia kuandaa miradi midogo midogo ambayo haina tija?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyoendelea kufuatalia suala la matumizi ya vyanzo nya uhakika kama Ziwa Tanzanyika. Wizara tumejipanga kuona kwamba maziwa yote tunakwenda kuyatumia tukiamini tunakwenda kutatua tatizo hili la maji na tutamtua ndoo mwanamama kichwani kama ambavyo Mheshimiwa Rais anatutaka na tumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kutupa fedha Wizara ya Maji. Hivyo, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi tuko katika kufanya usanifu ili kuona mwaka 2022/2023 matumizi ya maji makuu kama vyanzo nya maji nya uhakika yaweze kufanyika.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Yahya Mhata.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii ya maji inayokuba mji wa Mpanda inafanana sana na changamoto ya maji katika jimbo langu Nanyumbu. Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitumia takribani shilingi bilioni moja kujenga bwawa katika kata ya Maratani ili vijiji nya Lipupu, Maratani. Mchangani A na Malema viweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu haukufanikiwa na Waziri mwenye dhamana alifika katika jimbo langu na kuahidi kutoa kuchimba visima viwili katika kila kijiji hivi nilivyovitaja.

Je, ni lini ahadi hii ya Mheshimiwa Waziri itatekelezwa ili wananchi katika jimbo hili waweze kunufaika na hii ahadi ya Mheshimiwa Waziri? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ni deni na kwa sababu ameahidi Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Mbunge ninakuhakikisha mgao ujao visima vitakuja kuanza kuchimbwa fedha italetwa.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Daniel Awack, ajiandae Mheshimiwa Amar.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika Mji wa Karatu tuna bodi mbili za maji, Bodi ya *KARUWASA* inauza maji kwa shilingi 1,700 kwa *unit*, Bodi ya *KAFIWASU* inauza maji kwa kwa *unit* 3500. Sasa ni lini Serikali itaweza kuweka bei ya uwiano katika Jimbo la Karatu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Karatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi gharama za kulipia maji zimekuwa zikifanyiwa marekebisho kila inapobidi kwa kuzingatia uendeshaji wa mradi wa maji wa eneo husika. Hivyo, kwa Jimbo la Karatu nao mchakato unaendelea na tunaamini kabla ya mwaka huu wa fedha kukamilika basi bei hizi zitakuwa rafiki na itakuwa kwa manufaa zaidi ya wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amar, ajiandae Mheshimiwa Deo Sanga.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza nianze kumpongeza Waziri wa Wizara ya Maji pamoja na Naibu kwa kuendelea kutukamilishaia mradi wetu ambao ulikuwa unaitwa ni mradi kichefuchefu wa Wilaya ya Nyang'hwale kutoka Nyamtukuza kwenda Bukwimba kwamba sasa hivi maji hayo tayari tumeanza kuyatumia, lakini kuna tatizo moja maji yale si safi na salama, hawajajenga chujio la maji.

Je, Serikali inatua hidi nini kwenda kujenga hilo chujio la maji ili tuweze kupata maji safi na salama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amar kutoka Nyang'hwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan huu mradi ulikuwa kichefuchefu lakini kwa sasa hivi kama alivyokiri mwenyewe Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake za ufuatiliaji pamoja na mashirikiano mazuri sasa hivi maji yanatoka. Kuhusiana na chujio ni hatua inayofuata na yenye we pia tutakuja kukamilisha. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Deo Sanga.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutupatia fedha za mradi wa maji katika cha Ibatu.

Swali, kwa kuwa mkandarasi aliyopewa mradi huu kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Ibatu mpaka sasa ameingia mitini, hakuna shughuli zinazoendelea. Nini mpango wa Serikali na kwa nini Serikali isiweke mkandarasi mwingi au ikafanya kazi wizara yenye we?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga kuhusiana na mradi wa Ibatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumefuatilia huyu mkandarasi *Farbank Company* na tayari tumewaagiza mameneja ambao wako pale Njombe wanafanya kazi. Kwa sasa hivi mkandarasi amerejea kazini siku hizi mbili, lakini tumempa muda wa maangalizo kwa wiki mbili na baada ya hapo basi sheria itafuata mkondo wake.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Margaret Simwanza, Mbunge wa Urambo.

Na. 32

Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria Wilaya ya Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza: -

(a) Je, ni lini Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria Wilaya ya Urambo utaanza ili kutatua tatizo la maji katika Wilaya hiyo?

(b) Je, ni lini Serikali itachimba mabwawa katika Kata za Uyumbu na Kalemela hasa ikizingatiwa kuwa maombi yalishawasilishwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Urambo ni wastani wa asilimia 40. Katika kuboresha huduma hiyo, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 inatekeleza miradi ya Itibulanda na upanuzi wa mradi kutoka Itibulanda kwenda Nsenga. Miradi hiyo

inahusisha ujenzi wa matanki mawili yenyewe ujazo wa lita 50,000, vituo 13 vya kuchotea maji na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometra 17.6. Miradi hiyo itaongeza uzalishaji maji wa lita 32,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha huduma ya maji katika Kata za Uyumbu na Muungano, Serikali imepanga kujenga mabwawa mawili ya Kilemela kata ya Muungano na Izimbili kata ya Uyumbu. Mabwawa hayo yatahudumia jumla ya vijiji vya 22 na mkandarasi wa ujenzi wa bwawa la Kilemela atapatikana mwezi Aprili, 2022 Kwa upande wa bwawa la Izimbili kazi ya usanifu inaendelea na itakamilika mwezi Juni, 2022. Ujenzi wa mabwawa hayo utafanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, Mji wa Wilaya ya Urambo unatarajiwa kupata huduma ya maji kupitia Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28 ambapo chanzo cha maji kitakachotumika ni Ziwa Victoria. Taratibu za upatikanaji wa wakandarasi zimekamilika mwezi Desemba, 2021 hivyo utekelezaji utaanza ndani ya mwaka wa fedha 2021/2022.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na wananchi wa Urambo wana imani na Wizara hii inafanya kazi kubwa, lakini kwa leo naiomba Serikali itoe kauli hapa. Lini maji haya yanafika Urambo kutokea Tabora ambapo yameshafika kutoka *Lake Victoria*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la ngongeza la Mheshimiwa Margaret Sitta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema lini mradi utaanza kutekelezwa, kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha, mradi utaanza kutekelezwa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Tunaendelea Mheshimiwa Shamsia.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Serikali ilianza mpango wa kulipa fidia wananchi wa maeneo yaliyozunguka Mradi wa Mto Ruvuma, sasa nataka kujua kwa nini Serikali inakwama kuendeleza mradi huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fidia ilishaanza kulipwa na itaendelea kumaliziwa ndani ya mwaka huu wa fedha, lakini mradi huu wa Mto Ruvuma ni katika ile miradi yetu ya kimkakati ndani ya Wizara kuona kwamba vinakuwa nyanzo vya kudumu kwa kutoa huduma ya maji kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kitandula.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; hali ya upatikanaji maji Wilaya ya Mkinga kwa sasa ni mbaya sana. Hivi ninavyozungumza mabwawa takribani matano yamekauka, tumeanza kuona dalili za ugonjwa wa homa ya matumbo. Sasa Wizara ilituma wataalam kufanya usanifu wa mradi mkubwa wa kutoa maji Mto Zigi kwenda mpaka Horohoro ambapo kazi hiyo inakamilika kesho. (*Makofii*)

Je, Serikali iko tayari kwa udharura huu kuhakikisha inaharakisha mchakato wa kupata wakandarasi, ili mradi ule uanze kushughulikiwa haraka iwezekanavyo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kitandula, Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu maji ni uhai na sisi kama Wizara ya Maji hatupendi kuwa kikwazo na kusababisha milipuko ya magonjwa. Kwa kutambua hilo kama Wizara tunamshukuru Mheshimiwa Rais aliongoza dua na sasa hivi mvua zimeanza kunyesha vizuri, mabwawa yaliyokauka tunayatarajia yarudi katika hali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika usanifu huu unaoendelea ambao tunautarajia ukamilike kesho, tutaharakisha kuona kwamba lile bwawa ambalo linafanyiwa usanifu na maeneo yale ya Mkinga yote tunakwenda kuyafanya kazi kwa haraka. Ninawaagiza ile timu iliyotumwa kule na Mheshimiwa Waziri ifanye kadri ya maagizo ya Mheshimiwa Waziri yaliyopo ili kuona tunaharakisha jambo hili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Dkt. Pius Chaya.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Manyoni Mashariki tuna mradi mkubwa wa shilingi bilioni 10 unaojulikana kwa jina la Kintinku-Lusilile. Kwanza naishukuru Serikali mpaka sasa hivi tayari chanzo cha maji kimepatikana. Lakini ningependa kusikia majibu ya Serikali ni lini sasa mkandarasi wa kusambaza maji, katika mradi huo katika Kata za Kintinku, Maweni na Makutupora ataanza kazi? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ni lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Pius Chaya; ni kweli mradi huu una vijiji 11 na tayari vijiji vitatu vimeshaanza kufanyiwa kazi na wiki ijayo tunatarajia kusaini mkataba wa kukamilisha vijiji nane vilivyobaki na tayari tumetenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 3.3 ili mradi huu uweze kuendelea katika utekelezaji wake. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda wa kuuliza swali la nyongeza.

Mji wa Mpanda ni kati ya miji 28 ambayo inatakiwa kupewa mradi wa maji; ni lini mradi huu utaletwa Mji wa Mpanda? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Swali fupi la Kibunge kabisa. Hongera sana ndio maswali yanayotakiwa namna hivyo. Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapufi kutoka Mpanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya miji 28 tutarajie itaanza ndani ya mwezi huu wa pili au wa tatu kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Polepole.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za Kitafiti zinasema kila mwaka tani milioni tatu za udongo zinaingia katika Ziwa Victoria na kulipunguzia Ziwa hilo kina cha maji. Serikali ina mpango gani na iko katika hatua ipi ya kutekeleza *National Water Grid* au mtandao wa maji wa kitaifa kutoka Kusini, Kaskazini, Magharibi ili kuweza kupunguza *pressure* katika Ziwa Victoria? Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Polepole kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna hii changamoto ya matope kuingia katika vyanzo vyetu vya maji na sisi kama Wizara tuna ofisi zetu za mabonde zinazoshughulika na kazi hizi na tayari Mheshimiwa Waziri amewaaagiza. Hivyo, tayari hili linafanyiwa kazi kuona kwamba tunaendelea kutunza na kuvilinda vyanzo vyetu vya maji. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mtenga.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nataka nielewe sisi kule kwetu Mtwara nimechimbiwa visima vitatu katika Jimbo langu, lakini takriban mpaka sasa hivi karibu miezi minne inakimbilia na mvua zinaanza kunyesha na visima vile tayari vimeshaanza kuziba.

Ni lini sasa visima vile vitamaliziwa kwa taratibu zingine za upatikanaji wa maji? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mtenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mwenyezi Mungu; Mheshimiwa Rais alitupatia fedha na visima vimechimbwa, kinachofuata ni mtandao wa usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa agizo kwa Mameneja wa Mtwara wafanye kazi haraka iwezekanavyo ndani ya mwezi mmoja, waweze kuona kwamba utaratibu wa mwendelezo wa visima hivi inaweza kufanyika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Martha Festo Mariki, kwa niaba yake Mheshimiwa Kabati. (*Makofi*)

Na. 33

**Ujenzi wa Barabara za kuunganisha Mkoa wa Katavi
na Mikoa ya Jirani**

MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. MARTHA F. MARIKI
aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara za kuunganisha Mkoa wa Katavi na Mikoa ya jirani utaanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG.
GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya barabara za kuunganisha Mkoa wa Katavi na mikoa jirani ya Kigoma, Rukwa na Tabora ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuunganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma ambapo ujenzi wa barabara ya Mpanda – Ifukutwa - Vikonge yenye urefu wa kilometra 37.65 umekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 sehemu ya barabara ya Vikonge – *Mishamo Junction* yenye urefu wa kilometra 62 imetengewa shilingi milioni 3,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali kuitia *TANROADS* iko katika hatua za mwisho za mchakato wa zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mikoa ya Katavi na Rukwa, ujenzi wa sehemu za Sumbawanga – Kanazi urefu wa kilometra 75, Kanazi – Kizi – Kibaoni kilometra 76 na Mpanda – Sitalike kilometra 36.5 kwa kiwango cha lami

umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 4,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kibaoni – Sitalike yenye urefu wa kilometra 71. Serikali kupitia *TANROADS* iko katika hatua za mwisho za mchakato wa zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa Mikoa ya Katavi na Tabora, utekelezaji wa barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda yenye urefu wa kilometra 359 ni kama ifuatavyo; Tabora – Sikonge yenye urefu wa kilometra 30 ujenzi umekamilika; sehemu ya Usesula – Komanga yenye urefu wa kilometra 108 na barabara ya kuingia Mji wa Sikonge yenye urefu wa kilometra 7.5; sehemu ya Komanga – Kasinde yenye urefu wa kilometra 108 na barabara ya kuingia Mji wa Inyonga kilometra 4.8; sehemu ya Kasinde – Mpanda kilometra 108 na barabara ya kuingia Mji wa Urwira yenye urefu wa kilometra 3.7 ujenzi wake umekamilika. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa maswali madogo mazuri ya nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini mradi wa barabara inayounganisha Jimbo la Iringa Mjini, Jimbo la Kalenga na Jimbo la Kilolo utakamilika? Kwa sababu mradi huo ni wa siku nyingi sana na wakati wa mvua wananchi wanapata mateso makubwa na barabara hiyo ni ya kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; ni lini mradi wa barabara ya Msembe inayokwenda *Ruaha National Park* utakamilika? Kwa sababu barabara hiyo pia ni ya kiuchumi na inakosesha mapato makubwa sana kwa Serikali kwa kuingiza mapato ya watalii wa ndani na wa nje. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na jibu la barabara ya *Ruaha National Park*; barabara hii ipo kwenye bajeti na iko kwenye taratibu za manunuzi. Hali kadhalika barabara ya lringa kwenda Kilolo inaendelea kujengwa na tuna hakika kadri fedha zitakavyopatikana barabara hii ni azma ya Serikali iweze kukamilika kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jerry Silaa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa inayofanya kwenye miundombinu ya barabara. Tarehe 1 Februari Daraja la Tanzanite limeanza kutumika pale Dar es Salaam. Kwa niaba ya watu wa Dar es Salaam tushukuru sana na nikuombe Kamati za mwezi Machi zifanye ziara Dar es Salaam mpate kupiga picha pale kwenye daraja la kisasa kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hali ya barabara kwenye Jimbo la Ukonga inaweza isitofautiane sana na kule Katavi kwa Mheshimiwa Martha aliyeuliza swali la msingi. Iko barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (kilometra 14.7) ambayo nishukuru sana Serikali imeshajengwa kwa kilometra 3.2 na kwenye llani ya Uchaguzi ukurasa wa 78 inaeleza wazi kukamilisha ujenzi wa barabara kwa kilometra 11.5 kutoka eneo la Kivule Mwembeni – Fremu Kumi – Msongola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inahudumia watu wengi na hali yake ni mbaya mpaka inasababisha...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jerry swali.

MHE. JERRY W. SILAA: ...mpaka inasababisha Mbunge siwezi kufanya ziara Kivule bila kuwa na mabaunsa wa kunilinda kutokana na kero kubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali inieleze, haionti inahitajika jitihada ya dharura kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa kilometra hizi 11.5 kama inavyosema kwenye llani ya Uchaguzi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee pongezi kwa niaba ya Serikali kutoka kwa Mbunge kwa kazi ambazo Serikali inaendelea kuzifanya, shughuli za miundombinu na ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga kwamba barabara ya Banana – Kitunda – Msongola kama ilivyoainishwa kwenye llani, lakini pia iko kwenye mpango wa Wizara kujengwa kwa kiwango cha lami na Serikali ina mpango wa kukamilisha barabara hii na ndiyo tayari kwanza tumeshakamilisha kilimeta 3.2 na hizo kilometra zilizobaki tunahakikisha kwamba tutazikamilisha ili wananchi waweze kupata huduma sahihi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gwajima.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya barabara za Katavi yanafanana sana na matatizo ya barabara ya Kawe. Nataka kuuliza swali dogo kwa Mheshimiwa Waziri; barabara ya Bagamoyo – Tegeta imejengwa hapo katikati haina mitaro kabisa na matokeo yake inasababisha mafuriko kwenye maeneo ya Basihaya, *DAWASCO* na Boko; ni lini sasa

Mheshimiwa Waziri utakwenda pamoja na mimi uone jinsi ambavyo *TANROADS* wamejenga bila mtaro kabisa na inasababisha mafuriko ambayo yanahatarisha maisha ya wananchi? Ni lini Mheshimiwa Waziri?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ni lini? Mpe tarehe, huna haja ya kusema mambo mengi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Askofu Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie mara baada ya kumalizika kwa Bunge tutaambatana naye kwenda kutembelea barabara hii. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kiswaga.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya heshima na mimi kuuliza swali la nyongeza. Lakini dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Ritta ameshauliza, ilikuwa ni ile barabara ya kwenda Msembe. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu. Mheshimiwa Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza, lakini pia niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuweka jiwe la msingi barabara ya mwendokasi ya Mbagala, kutoka Bendera Tatu kwenda Mbagala mambo ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza; ni lini sasa Serikali itakamilisha barabara ya kutoka Mbagala Kokoto mpaka kwenda Kongowe kupunguza msongamano wa magari na kero kubwa ya kupoteza muda katika eneo la Mbagala Rangi Tatu? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu, jiandae Mheshimiwa Mdee.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ni muhimu sana na imeainishwa kukamilishwa kwa kiwango cha lami, lakini itajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha na kwa kuwa tuko kwenye kipindi cha bajeti basi tutaangalia ili iweze kupangisha bajeti kwa mwaka ujao wa fedha. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Sanga. *Sorry,* Mheshimiwa Sanga halafu Mheshimiwa Mdee.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Lupila kuelekea Kipengere ni barabara ambayo inaunganisha Wilaya za Ludewa, Makete na Wanging'ombe na tumeiombea kibali kwenye RCC cha kupandishwa hadhi ya TANROADS, hadi leo takribani miaka mitatu imepita.

Je, ni lini Wizara itatoa kibali barabara iwe chini ya TANROADS ili iweze kujengwa na kupitika kwa uhakika kwa sababu wananchi wangu wanateseka sana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote ambazo zinahudumiwa na TAMISEMI kwa maana ya TARURA zina utaratibu wake. Naomba kama imefanyiwa tathmini

inawezekana imeshindwa kukidhi viwango, lakini tunaomba Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuonane ili tuweze kuona ni kitu gani kinakwamisha barabara hii kama inakidhi viwango isiweze kupandishwa hadhi na kuhudumiwa na TANROADS. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa Mbunge wa Kawe, mwaka 2015-2020 barabara ya Chuo cha Ardhi – Makongo Juu – Goba ilikuwa ina changamoto kubwa sana, tukafanikiwa kujenga kipande kutoka Goba mpaka Makongo Juu. Ilivyofika mwaka 2020 kipande cha Makongo Juu kwenda Chuo cha Ardhi akapatikana mkandarasi ambaye ikasemekana angejenga ndani ya mwaka mmoja. Sasa hivi ni mwaka wa tatu toka mwaka 2020 mpaka 2022 mkandarasi allyeko anasuasua, sasa sijui tatizo ni mkandarasi ama tatizo ni ufuatilaji.

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri wa Ujenzi aniambie ni lini kipande cha barabara cha Makongo Juu kwenda Chuo cha Ardhi kitakamilika na kwa viwango vyote? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu. Jiandae Mheshimiwa Kwagilwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Halima Mdee kwamba barabara hii ambayo inajengwa na anasema inachukua muda nimhakikishie kwamba kutoka hapa nitahakikisha nafuatilia nijue tatizo ni nini na nitatoa majibu kwa nini barabara hii imechukua muda mrefu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kwagilwa, ajiandae Mheshimiwa Tarimba.

MHE KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. kama ilivyo kwa Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Tanga haujaunganishwa na Mikoa miwili; Morogoro na Manyara. Barabara ya Handeni – Mziha – Turiani na barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto – Kondoa – Singida; ni lini Serikali itakamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa barabara hizi mbili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayoanza Handeni kwenda Kiberashi hadi Kwamtoro taratibu zipo zinaendelea kwa kuanza na kilometra 50 na ziko kwenye hatua ya manunuzi; na barabara ya Handeni – Turiani upande wa kwenda Turiani barabara inaendelea kujengwa na bado hatujakamilisha kwa sababu ya upatikanaji wa fedha, lakini tayari nayo tumeshaanza kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, ni matumaini ya Serikali kwamba barabara zote ziko kwenye mpango na zitakamilishwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Tarimba, jiandae Mheshimiwa Mwenisongole.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini la pili, nikupongeze wewe pamoja na Wabunge wote wapenzi wa *Simba Sports Club* kwa kuonja ushindi angalau jana; matarajio yetu mtaendelea na utaratibu huo ambaa mmeuanzisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu; naomba nipate kauli ya Serikali juu ya matumizi ya barabara wanazozijenga Serikali, hasa barabara ya mwendokasi pale Dar es Salaam na hususan katika Jimbo langu la Kinondoni. Matumizi ya barabara zile yamekuwa mabaya sana, pikipiki zinapita, magari binafsi yanapita, magari ya Serikali yanapita, hali ambayo inasababisha ajali nyingi sana.

Ni nini kauli ya Serikali pamoja na vyombo vyake kuhakikisha kwamba tabia hii ya kutumia vibaya barabara zinazojengwa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tarimba umeshaeleweka; Mheshimiwa Waziri.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, lakini na la kwanza umenielewa Mheshimiwa, la pongezi. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tarimba, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alichokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwa na kutokutumia vizuri barabara hizi za mwendokasi na inawezekana ni kwa sababu tu hizi barabara kwetu ni mpya. Lakini naomba nitumie nafasi hii kuwalishwa wananchi wa Tanzania kwamba zile barabara zimewekewa alama na zina matumizi yake. Barabara ya mwendokasi ni ya mwendokasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nitumie nafasi hii kuhakikisha kwamba watumiaji wote wa barabara hizi za Dar es Salaam ambapo mwendokasi unapita basi wazingatие sheria ili tuisababishe ajali na matatizo mbalimbali kwa watumiaji wa barabara. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwenisongole.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa hii nafasi ya kuiliza swali la nyongeza.

Barabara ya Mlowo – Utambalila – Kilyamatundu inaunganisha Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Katavi, na ni barabara ya pili kwa ukubwa ndani ya Mkoa wetu wa Songwe. Kwa sasa hii barabara maeneo ya Itewe pale Itaka pameharibika na imesababisha kero kubwa kwa wananchi wa Songwe, Mbozi na mikoa ya jirani. Ni nini kauli ya Serikali kuhusu matengenezo ya haraka yanayohitajika ili kuinusuru barabara hiyo na hizi mvua zinazoendelea?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mlowo – Itaka – Kilyamatundu ni barabara muhimu sana kwa Mkoa wa Songwe ambayo inaunganisha na Mkoa wa Rukwa; na kwa kuwa hiki ni kipindi cha mvua, naomba pia nitumie nafasi hii kuwajulisha na kuwaelekeza Mameneja wote wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba kila kunapotokea changamoto kwenye barabara ambazo tunazihudumia basi wazishughulikie mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nitumie nafasi hii kumuagiza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Songwe kesho afike eneo la Itaka, Kijiji cha Itewe kwenye changamoto ili aweze kutatua hiyo changamoto, na mimi mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Mbunge tuweze kupata majawabu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mama Malecela kwa upendeleo maalum.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Novemba nilikuwa kwenye kata yangu inaitwa Lugulu, Mheshimiwa Naibu Waziri akanifuata kule akaja akaniambia kwamba barabara yangu ya Mkomazi – Kisiwani Same yote inatangazwa kujengwa moja kwa moja.

Sasa ninapenda Mheshimiwa Waziri awatangazie wananchi wangu ndani ya Bunge kile alichoniambia kule Lugulu ili wananchi wangu wasikie. Nashukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru na nimpongeze Mheshimiwa Anne Kilango kwa kufuatilia maendeleo ya barabara za jimbo lake; na ni kweli nilikwenda kwenye jimbo lake na yalikuwa ni maagizo pia ya Kiti kwamba niende nikatembelee barabara za Same.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizi zote ambazo tumeziongelea sana ziko kwenye hatua mbalimbali za manunuzi ikiwepo na barabara aliyoitaja ya Kisiwani – Mkomazi. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano; Mheshimiwa Subira Mwaifunga.

Na. 34

Tatizo la Mawasiliano ya Simu Jimbo la Tabora Mjini

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA aliuliza: -

(a) Je, ni lini Serikali itafanya maboresho ya mawasiliano ya simu katika Jimbo la Tabora Mjini hususan kwenye kata za pembezoni?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka minara ili kuondoa changamoto hii hasa katika kata ya Itetemia ambayo ina changamoto kubwa ya mawasiliano?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum - Tabora, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilifanya tathmini katika Jimbo la Tabora Mjini na kubaini kuwa kata 12 za pembezoni zilikuwa zinahitaji wa kufanyiwa maboresho ya huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imefikisha huduma za mawasiliano ya simu katika kata tatu za pembezoni ambazo ni Kabilia - mtoa huduma ni Halotel; Kalunde na Uyui - mtoa huduma ni Vodacom ndio wamefikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo hayo yenye teknolojia ya 2G pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ipo katika maandalizi ya awali ya kutangaza zabuni ya kuboresha miundombinu ya minara iliyopo ili iweze kutoa huduma za mawasiliano zenye kutumia teknolojia ya 2G/3G na 4G. Aidha, ujenzi wa minara katika teknolojia ya 2G/3G na 4G unaendelea katika kata tatu za Ndevela, Tumbi pamoja na Itetemia kupitia mtoa huduma Halotel.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna changamoto ya mawasiliano katika Kata ya Itetemla; Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iliitangaza kata ya Itetemla katika zabuni ya awamu ya nne na kupata mtoe huduma ambae ni Kampuni ya Simu ya Halotel kwa ajili ya kifikisha huduma za mawasiliano ya simu katika kata hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mnara huo wa simu upo katika hatua za mwisho na unatarajiwa kuanza kutoa huduma kabla ya mwezi Julai, 2022 na utakuwa na teknolojia ya 2G/3G na 4G.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; pamoja na majimu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amekiri Jimbo la Tabora Mjini lina sura mbili yaani Kata za Mjini na Kata za Vijijini; changamoto ya mawasiliano ni kubwa sana katika kata za mjini na kata za pembezoni. Kata za vijijini zina vijiji zaidi ya 41, asilimia 75 ya vijiji hivyo haina mawasiliano kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema kwamba wamepeleka mawasiliano katika Kata za Kabilia na maeneo mengine, lakini Kabilia ni pale *center* ndipo ambapo unapata mawasiliano; lakini kwenye Vijiji vya Igosha, Umanda na vijiji vingine havina mawasiliano kabisa.

Je, Mheshimiwa Waziri ni kwa asilimia ngapi ya vijiji vya kata za pembezoni ambazo tayari mmeshapeleka mawasiliano hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata za Mjini ukiwa katika Kata za Malolo, Ng'ambo na Kidongo Chekundu hupati mawasiliano kabisa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa uliza swali tafadhalii.

MHE. HAWA S. MWAIIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti nimtajie kata ambazo zina changamoto na mawasiliano ili aweze kujibu vizuri. Katika kata hizi tatu za Kidongo Chekundu, Ng'ambo na malolo hakuna mawasiliano kabisa tunapokuwa katika kutembelea wananchi maeneo hayo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha pia mawasiliano katika Kata za Mjini ambazo hazina mawasiliano? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum - Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala la mawasiliano katika Mji wa Tabora na Serikali inakiri kabisa kwamba Mji wa Tabora ulikuwa na changamoto kubwa ya mawasiliano. Lakini mpaka hapo anaposema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kabisa kwamba vijiji vingi havikuwa na mawasiliano, lakini mpaka sasa kuna vijiji vingi ambavyo vimeshapata mawasiliano ambapo tunaamini kabisa kwamba katika utekelezaji wa mpango wa mwaka mmoja mmoja na katika utekelezaji wa miaka mitano tunaamini kabisa kwamba tutakuwa tumefikia katika hatua nzuri kabisa ya kutatua changamoto ya mawasiliano katika kata za pembezoni katika Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile upande wa kata za mjini; kata za mjini changamoto yake ni moja, ni kwamba kulikuwa na minara ambayo tayari ilikuwa imeshaanza kuzidiwa na tayari Serikali imeshatenga takribani shilingi bilioni 7.6 ambapo tunakwenda kufanya *upgrade* ya minara takribani 380 nchi nzima; na Tabora Mjini ikiwa sehemu mojawapo ya minara ambayo inakwenda kufanyiwa kazi. Lakini pamoja na hivyo kuna minara ambayo ilikuwa inatoa

huduma ya 2G maana yake kwamba hapakuwa na uwezekano wa kupata *internet* lakini katika mpango huu huu Tabora Mjini tumeiweka katika mpango kabambe ambapo na Mheshimiwa Mbunge tutamshirikisha wakati tukifika Tabora kwa ajili ya kutatua hii changamoto ambayo wananchi wa Tabora wamekuwa wakilalamikia kwa siku nyingi. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ndaisaba.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, lakini pia na kwa kutoa fursa nyingi kwa Waheshimiwa Wabunge kuuliza maswali mengi ya nyongeza, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kujenga minara tisa ya mawasiliano kwenye Jimbo la Ngara. Naomba kuiuliza Serikali ni lini ujenzi huu wa minara tisa utaanza ili kutatua changamoto ya mawasiliano kwenye jimbo la Ngara? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali ilitangaza kujenga minara tisa katika Jimbo la Ngara katika awamu iliyopita iliyokuwa imetangazwa. Lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, mwezi huu anakwenda kusaini mkataba wa ujenzi wa minara 90 ambayo ni pamoja na minara ambayo itakuwa hapo katikati Jimbo la Ngara.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na subira ili Mheshimiwa Waziri akishakamilisha jambo hili tayari utekelezaji utaanza mara moja. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea muda wetu umekwisha na maswali bado ni mengi. Wizara ya Katiba, Mheshimiwa Getere.

Na. 35

Mikataba ya Miradi Mikubwa Nchini Kuletwa Bungeni

MHE. CECIL D MWAMBE K.n.y. MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

(a) Je ni lini mikataba ya miradi mbalimbali ya migodi ya madini, ujenzi wa Bandari Bagamoyo, ujenzi wa Reli (*SGR*), ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Bomba la Mafuta na Mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam italetwa Bungeni ili kupata ufahamu wa miradi hiyo?

(b) Je, katika mikataba hii ni mingapi imewahi kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali?

MWENYEKITI: Si ultakiwa ungoje uitwe kwanza! Haya Mheshimiwa Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za mikataba ya ujenzi wa Reli ya *SGR*, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Migodi ya Madini, Bomba la Mafuta na Mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kwa nyakati tofauti Taasisi na Mashirika yanayosimamia miradi hii yamekuwa yakiwasilisha kwenye Kamati za Kudumu za Bunge taarifa za mikataba ya miradi hiyo. Aidha, Kamati zina mamlaka kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kupata taarifa zozote kuhusiana na mikataba ya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, miradi hii imekuwa ikikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaani *CAG*. Kwa kuwa baadhi ya miradi Serikali inamiliki kwa asilimia 100 na mingine Serikali ni mbia, hivyo taarifa zake huwasilishwa katika Bunge lako tukufu kupitia Ripoti ya *CAG*. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Sura ya Tano na Sita inabainisha kwa kina taarifa ya ukaguzi ya miradi ya ujenzi wa Reli *SGR*kwa *Lot. 1* na *Lot. 2* na Mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere. Aidha, mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam umekuwa ukifanyiwa ukaguzi wa kawaida kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumuarifu Mheshimiwa Mbunge na pia Bunge lako tukufu kuwa Bunge limekuwa likipokea taarifa za mikataba na Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama nilivyoeleza hapo juu. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka mwaka jana mwishoni, Mheshimiwa Spika aliunda Kamati Maalum kabisa ambayo ilikuwa ni Kamati ya Viwanda na Biashara pamoja na Kamati ya Bajeti na tulikaa kwa nia ya kutaka kupitia mambo mbalimbali kwa sababu tulipokea taarifa za malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusiana na bei kubwa za *stamp* za kielektroniki. Lakini nimesimama hapa nikwambie tu kwamba pamoja na mazungumzo yale Serikali au *TRA* waliendelea kusaini mkataba huo ambao umekuwa wa kinyonyaji kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimuulize Waziri wetu wa Katiba kwamba je, yupo tayari sasa kuleta mkataba katika ya *SICPA* na Serikali unaohusisha masuala ya *stamp* za kielektroniki ili tuweze kuwasaidia wananchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, pamoja na hiyo mikataba mingi uliyoisema na sisi kama Wabunge wengi tunatamani kujifunza na wengine siyo wahudhuriaji kwenye

Kamati hizo ulizozitaja. Hauoni sasa ni wakati mikataba hiyo kwa mfano hiyo *SGR*, mikataba wa Bandari ya Bagamoyo, mikataba wa gesi wa kule Mtwara na mingine mingi kuwa wazi kwa Wabunge wote kuisoma na kupata uelewa wa kina kuweza kuishauri Serikali? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikanza na swali la nyongeza la kwanza la Mheshimiwa Mwambe hili linalohusu *stamp*, nadhani tutafanya mawasiliano na taasisi inayohusika ili tuweze sasa kujiweka sawa katika eneo hili ambalo limeonesha mashaka ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kuhusu suala la kuwasilisha mikataba katika Bunge lako tukufu kama nilivyoeleza mwanzo, mikataba hii huwa inapita kwenye Kamati kwa sababu ndiyo taratibu zilizowekwa. Kama Bunge lako tukufu litataka mikataba ufikishwe mbele ya Bunge lote basi maamuzi yanatoka kwenye Kamati baada ya kupitia zile taarifa zinazowasilishwa. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Wizara ya Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Asia Halamga

Na. 36

**Wakandarasi wa Tanzania Kujenga Mnara wa
Mwalimu Nyerere – Umoja wa Afrika**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MHE. ASIA A.
HALAMGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wakandarasi wa Tanzania wanapata fursa ya kujenga Mnara wa Mwalimu Nyerere katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika hasa ikizingatiwa kuwa Serikali ya Tanzania ndio inasimamia ujenzi wa mnara huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni Na. SADC/NYERERE ST/02 ilipotangazwa kati ya mwezi Mei na Julai, 2021 ilitoa fursa sawa kwa wakandarasi wote kutoka nchi Wanachama wa *SADC*. Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa ilichukua jitihada za kuwatangazia na kuwahamasisha wadau wote nchini kupitia Shirikisho la Sanaa za Ufundu na Idara za Sanaa za Vyuo Vikuu mbalimbali nchini illi wenyewe vigezo vilivyoainishwa kwenye zabuni waweze kuomba kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu wapo wakandarasi wa Kitanzania walioomba kazi hii sambamba na wenzao kutoka mataifa wanachama wa *SADC*. Hivi sasa *SADC* imekamilisha uchambuzi wa nyaraka na muda wowote mshindi atatangazwa baada ya kusaini mkataba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ng'wasi.

MHE. NG'WASI D. KAMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa ujenzi huu maazimio ya kikao hiki yaliuweka kusimamiwa na Serikali ya Tanzania na kwa kuwa ujenzi wa sanamu hii ya Baba yetu wa Taifa yatasaidia kutangaza utamaduni wa Tanzania na mchango mkubwa wa Baba yetu Taifa katika kupigania uhuru wa nchi mbalimbali za Afrika. Ningependa Serikali ituambie ni kwa nini tangu mwaka 2015 yalipopitishwa maazimio haya mpaka sasa ujenzi huu haujaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kwa kuwa maamuzi haya au maazimio haya ya kikao yalitoa kipaumbele kwa wakandarasi wazawa wa Tanzania kuwa wa kwanza kabisa kupewa *tender* hizi na kwa kuwa mwaka 2018 *tender* hizi zilipotangazwa ilionekana hakuna wasanii/vijana Watanzania wenye vigezo vya kutosha kimataifa kujenga sanamu hii. Basi Serikali ningependa ituambie ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inakuza ujuzi na uwezo wa wasanii wa Tanzania ili pale *tender* kama hizi zinapojitokeza kimataifa.

MWENYEKITI: Swali, swali, swali.

MHE. NG'WASI D. KAMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo swali hili.

Ningependa Serikali itueleze ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wasanii wa Tanzania pale ambapo *tender* hizi za kimataifa zinatangazwa tena wanajengewa uwezo ili nao wapate kushiriki kama Nchi zingine? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kamani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kamani kwanza amependa kufahamu kwa nini *delays*. Nipende kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba mchakato huu wa kujenga sanamu ya Baba wa Taifa Ethiopia Addis, ilikuwa ni wazo zuri sana kwa wakuu wa nchi za *SADC* kuipa heshima Taifa letu lakini kumpa heshima Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *delays* hizi zinatokana na mchakato; kwanza Kamati lazima ziundwe za kitaifa lakini pia kuititia Kamati hizo lazima zikae na familia ya Baba wa Taifa ili kupata *prototypes* zile ambazo zinahitajika tatu kabla ya ujenzi wa sanamu hii. Lakini pia *conditions* ambazo *SADC*

imetupa ni kwamba lazima picha ya Baba wa Taifa iwe ni enzi hizo miaka hiyo wakati anapigania uhuru wa Taifa hili.

Kwa hiyo michakato hii, pamoja na *conditions* mpaka sasa inaendelea vizuri lengo ikiwa ni kuhakikisha sanamu tutakayojenga pale Ethiopia iwe ni samanu ambayo inaakisi picha halisi ya Baba wa Taifa. Kwa hiyo, michakato hii inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lako la pili la Mheshimiwa Ng'wasi, ni kwa kiasi gani wasanii wetu tunawashirikisha na tunawajengea uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeza Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge kwamba mlitupitishia bajeti katika Bunge hili ya zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya sanaa na utamaduni. Kupitia mfuko huu Mheshimiwa Mbunge tukuhakikishie tutaendelea kuwajengea uwezo wasanii wetu, lakini kwa kuwa Tanzania tumepewa nafasi ya kusimamia ujenzi huu wa sanamu ya Baba Taifa, meneja wetu huyu aliyeteuliwa pia amepewa nafasi mbili ya kwenda na wasanii wetu Ethiopia waweze kuona kwamba wasanii wetu waweze kujua teknolojia hii ya Kwa hiyo, hii ni Wizara yetu tunalifanyia kazi kwa karibu kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa.

MWENYEKITI: Ahsante, Wizara ya Afya Mheshimiwa Midimu, kwa niaba.

Na. 37

Kuanza Ujenzi wa Kiwanda cha Vifaa Tiba – Simiyu

MHE. LUHAGA J. MPINA K.n.y. MHE. ESTHER L. MIDIMU
aliuliza:-

Mwaka 2018 Mkoa wa Simiyu ultienga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Vifaa Tiba vitokanavyo na malighafi ya pamba na utaratibu wa kuanza ujenzi

umeshakamilika, lakini kibali cha ujenzi toka Serikali kuu kimechukua muda mrefu.

Je, ni lini Serikali itatoa kibali kuruhusu ujenzi kuanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mifuko ya *WCF* na *NHIF* ilipanga kujenga kiwanda cha kuzalisha vifaa tiba vinavyotumia malighafi ya pamba chenye thamani ya shillingi bilioni 59.4. Wakati wa upembizi yakinifu wa awali ilionekana kutumia miundombinu tuliyonayo, kiwanda hicho kinaweza kujengwa kwa shillingi bilioni 8.4 na kuokoa shilingi bilioni 51.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya mwisho inamalizika mwishoni mwa mwezi wa pili ili kukutanisha mifuko husika na Serikali ya Mkoa wa Simiyu kupeana mwelekeo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpina.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasikitika sana kwa majibu haya yaliyotolewa na Serikali. Kipindi cha miaka minne toka mwaka 2018 mpaka leo Serikali inazungumzia suala la tathmini, inazungumzia suala la upembizi yakinifu, miaka minne! Wananchi wa Simiyu wamechoka na hizi danadana za Serikali, leo tunataka tuambiwe nini sababu zilizouzia mradi huu kujengwa ili tujue, kwa sababu huwezi kutuambia hadi miaka minne unazungumzia tathmini, unazungumzia upembizi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni nchi yetu imekuwa ikiagiza bidhaa za nguo kutoka nje ya nchi kutokana na ukosefu wa viwanda kama hivi, tunaagiza bidhaa za nguo

kutoka nje tunatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa za nguo nje ya nchi. Lakini pia wananchi wa Tanzania wanateseka kwa kukosa soko zuri la pamba kwa sababu ndani ya nchi hakuna viwanda na kugeuka kuwa soko la wakulima wa nchi zingine kwa kununua bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ajira zetu tunazi-*export* kila leo; Serikali ituambie ni lini Serikali itachukizwa na mambo haya na kuingia kwenye uwekezaji wa viwanda vya pamba ili wakulima wa pamba waweeze kupata bei nzuri na tuweze kunufaika na *valua addition* la zao la pamba? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mbunge kwa swali lake zuri la nyongeza na ni kweli akisikitika ana haki ya kusikitika, lakini kiukweli ilikuwa ni lazima taasisi yetu ya *TIRDO* ifanye upembuzi yakinifu wa kuhakikisha kwamba kinachokwenda kufanyika je, kinaweza kuleta manufaa tarajiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile ikumbukwe kwamba kuna mifuko kama mitano ambayo ilikuwa ichangie kwenye ujenzi huo; kwa maana ilikuwa kwanza ni kuhakikisha hii mifuko inakubaliana na *module operant* pamoja na kufanya hayo mambo mengine, lakini kimsingi ilionekana vilevile katika upembuzi yakinifu ndiyo maana utaona upembuzi wa kwanza ulionesha tunahitaji shilingi bilioni 59.4 kujenga. Lakini wakati wakifanya mchakato wakaona kwamba kuna uwezekano wa kuokoa hizo shilingi bilioni 51.

Sasa labda Mheshimiwa anasema ni lini tutamalizana na jambo hilo, labda Mheshimiwa Mbunge nikuombe kitu kimoja kabla ya tarehe 15 Machi, 2022 tayari kitaitishwa kile kikao ambacho kitaelezea muafaka wa hili jambo na Mheshimiwa Mbunge tutawaalika Wabunge wa Mkoa wa Simiyu ili tuweze kukubaliana *way forward* kwa pamoja.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea muda wetu umekwisha. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kawawa.

Na. 38

**Hatima ya Silaha zilizochukuliwa wakati wa
Operesheni Tokomeza – Namtumbo**

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwarudishia wamiliki halali silaha zao ambazo zilichukuliwa na Serikali wakati wa zoezi la Operesheni Tokomeza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO
NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2013, Serikali baada ya kuona matukio ya ujangili na uwindaji haramu umeongezeka hapa nchini, hasa kwenye hifadhi za Taifa na mapori tengefu, iliendesha Operesheni Tokomeza na lengo lake lilikuwa kuwasaka na kuwakamata majangili pamoja na silaha walizokuwa wakizitumia. Operesheni hiyo ilishirikisha *TAWA* pamoja na vikosi vya ulinzi na usalama na jumla ya silaha 1,579 zilikamatwa na mpaka sasa zinashikiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 7 Januari, 2017 Serikali kupitia Wizara za Kisekta ambazo ni Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Katiba na Sheria,

walikubaliana kwa pamoja silaha hizo zisirudishwe kwa wamiliki mpaka itakapofanyika tathmini ya hitaji la kuwarejeshea wamiliki wa silaha hizo. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana; kwa kuwa kulikuwa na wananchi ambao walipata silaha hizo kihalali na kwa kufuata taratibu zote na walikuwa wanazilipia kila mwaka na wenyewe walitii amri kwa kuzipeleka katika vituo vya polisi na sasa Serikali imeamua hivyo isiwarudishie. (*Makofi*)

Je, Serikali inaweza sasa kuwarudishia thamani ya gharama ya silaha zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa Jimbo la Namtumbo ni la wakulima na mashamba yao yamezungukwa na mapori yenye wanyama wakali na waharibifu na kwa kuwa Serikali awali dhamira yake iliwaruhusu kuwa na silaha hizo ili waweze kujilinda wao wenyewe na mali zao ambayo ni mashamba yao.

Je, Serikali sasa ina mpango gani mbadala wa kuweza kuwasaidia wakulima na wananchi hawa, kuepukana na adha wanayoipata ya kuharibiwa mazao yao na kuuawa na wanyama waharibifu na wakali? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Kawawa, lakini pia niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Namtumbo kwa kuendelea kuwa na subira kwa jambo hili. Wamesubiri kwa muda mrefu lakini

nataka niwaambie wananchi na Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali na lengo lake ni kulinda raia na malizao. Tunaposikia mahali kuna majangili, kuna majambazi, kuna magaidi, kuna watu ambao aidha wanataka ama wanafanya shughuli ama mambo ya uvunjifu wa amani, sisi kama vyombo vy'a ulinzi na usalama wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kutuliza na ikiwezekana kukamata kila kinachohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukitazama hili jambo suala la uchunguzi sio jambo la kusema kwamba tunafanya leo na kesho na silaha zimetajwa hapa katika jibu la msingi ni karibu 1,579. Lakini hazikukamatwa silaha tu kuna wahalifu waliokukamatwa na silaha hizi sio hizi silaha hizi tu kuna visu, kuna mapanga na nyinginezo. Nadhani wengi wenu mnakumbuka zile operesheni za Kibiti na nyingine.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake waendelee kuwa na subira. Serikali kupitia vyombo tunafanya uchunguzi kuhakikisha kwamba nani anayehusika na silaha ipi inahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ukiangalia katika masuala ya *investigation* sio jambo la kusema tunafanya leo, kesho tunapata majibu na ndio maana watu wengi walilalamika jambo linachukua muda mrefu kuchunguzwa kwa sababu tunataka tutende haki.

Lakini swalii la pili je, sasa Serikali ina mpango gani mbadala kusaidia kupunguza sasa hizi adha za wanyama pori. Nataka niendelee tena kumuambia Mheshimiwa Kawawa pamoja na wananchi wa Jimbo hili kwamba Serikali imekuwa ikifanya operesheni na misako mbalimbali ya kusaka hawa watu wahalifu. Lakini pia kuwasaidia kuerekana na madhara ya hawa wanyama pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kumekuwa kuna Jeshi letu hili linaloshughulika na masuala ya wanyama pori wanaweza pia tukawasaidia kupitia hili. Vilevile Serikali tumetoe namba maalum hasa kwa wale watu ambao

wanafanya kazi za kilimo na shughuli nyingine katika misitu, lengo na madhumuni ikitokea mtihani wowote waweze kutuambia. Tuendelee kuwaomba radhi na kuwaambia wananchi wasubiri jambo linafanyiwa ufuatiliaji. Nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete.

Na. 39

Ukarabati wa Jengo la Polisi Wete

MHE. OMAR ALI OMAR aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati jengo kongwe la Polisi Wete ambalo lipo katika hali mbaya?

(b) Je, ni lini Serikali itayatengeneza magari ya polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba ambapo kwa sasa ni gari moja tu linafanya kazi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI aliujibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Jimbo la Wete swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uchakavu wa jengo la Kituo cha Polisi Wete ambalo limejengwa mwaka 1973. Tathmini kwa ajili ya ukarabati ilifanyika mwaka 2021 na kubaini kwamba kiasi cha shilingi 52,760,000 kinahitajika ili kugharamia ubadilishaji paa, mfumo wa umeme, *ceiling board* pamoja na kupaka rangi. Hivi sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna magari ya polisi 12 na yanayofanya kazi ni magari matano na magari saba ni mabovu. Tayari magari hayo yameshafanyiwa tathmini ya ubovu na kubainika kuwa kiasi cha shilingi 44,254,000 kinahitajika kwa ajili ya ukarabati. Aidha, ukarabati huo utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Omar.

MHE. OMAR ALI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza ni kwamba kutokana na gharama ya fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo ambalo alisema kwamba ni chakavu lakini jengo hilo ni bovu kabisa.

Je, haoni Mheshimiwa Waziri kwamba kuna haja sasa ya kuambatana na mimi kwenda katika jengo hilo kwenda kujiona na kuona uhalisia wa gharama zinazohitajika katika kutengeneza jengo hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti swali langu la (b) ni kwamba kutokana na ongezeko la vitendo vya udhalilishaji na vitendo mbalimbali vya unyanyasaji wa wanawake na watoto katika eneo la Mkoa wa Kaskazini Pemba na magari ambayo yanatumika ni magari matano tu. Haoni kwamba kuna haja sasa ya kuweza kuongeza magari ya dharura kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vitendo hivi vinakomeshwa muda mfupi ujao? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar, Mbunge wa Jimbo la Wete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya miongoni mwa wajibu wetu mkubwa ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kuona kila jengo ikiwa nyumba za makazi, Kituo cha Polisi, mradi wowote ambao unashughulika na masuala ya Jeshi la Polisi ni wajibu wetu kwenda kuukagua. Nimwambie tu Mheshimiwa Omar kwa kushirikiana na wananchi wa Jimbo la Wete tupo tayari kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwenda kukagua na kuona na sio Wete tu, lakini maeneo yote ya Unguja na Pemba na Tanzania kwa ujumla. Ni sehemu ya wajibu wetu na tuko tayari kufanya hivyo na mimi niko tayari kuambatana na yeche.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine je, sasa si tupate hata gari kwa ajili ya doria na vitendo vyatuhalifu? Nimuambie tu Mheshimiwa katika bajeti ambayo tumeisoma ya mwaka 2021/2022 tulisema kwamba tuna jumla ya magari zaidi ya 300 ambayo yatakuja kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Nimuambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Jimbo la Wete tutaliangalia kwa jicho la huruma sana kuhakikisha kwamba gari hizo zinakwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha niwaombe radhi wale ambao hawakupata nafasi kutokana na maswali yalikuwa mengi kwenye maji na kwenye suala la barabara.

Sasa kuna matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni wawili wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Mbunge na Waziri wa Kilimo ambao ni Mkurugenzi Mkuu *TBL* - Ndugu Jose Moran na Mkurugenzi wa Uhusiano wa *TBL* - Ndugu Mesiya Mwangoka kutoka jijini Dar es Salaam, karibuni. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben ambao ni viongozi wa UVCCM Wilaya ya Handeni Mkoani Tanga, Ndugu Saidi Mbega na Ndugu Shaban Lugendo, karibuni (*Makofii*)

Wageni 31 wa Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Theofil Kisanji kutoka Mkoani Mbeya, wakiongozwa na Rais wa Serikali ya Wanafunzi Ndugu Mussa Mgwasa, karibuni (*Makof*)

Sasa namuita Waziri wa Nchi kutengua Kanuni.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkutano wa Sita wa Bunge umeanza tarehe 1 Februari, 2022 na umepangwa kumalizika tarehe 18 Februari, 2022;

Na kwa kuwa Kamati za Kudumu za Bunge, hazikupata fursa ya kufanya vikao vyake vyaa kawaida kwa wiki mbili kabla ya Mkutano wa Sita wa Bunge kuanza;

Na kwa kuwa ili shughuli zilizopangwa kufanyika katika Mkutano wa Bunge zifanyike, ni lazima kwanza zifanyiwe kazi katika ngazi ya Kamati;

Na kwa kuwa Kamati ya Uongozi katika Kikao chake cha tarehe 1 Februari, 2022 ilipitisha uamuzi kwamba, Vikao vyaa Kamati za Bunge vifanyike sambamba na Mkutano wa Bunge kwa utaratibu kwamba katika wiki ya kwanza Bunge lianze saa 3.00 asubuhi na kipindi cha maswali tu na kisha Vikao vyaa Kamati za Bunge viendelee;

Aidha, kwa wiki ya pili na ya tatu ya Mkutano ilikubalika kwamba Bunge lianze saa 8:00 mchana na muda wa asubuhi utumike kwa Vikao vyaa Kamati za Bunge;

Hivyo basi, ili kuwa na utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Sita wa Bunge, Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 34(1), (2), (3) na (4) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza Bunge kuanza saa 3:00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana na kurejea saa 11:00 jioni na kuendelea hasi saa 1:45 usiku, itenguliwe na badala yake kuanzia

Jumatatu tarehe 7 Februari, 2022 Bunge lianze saa 8:00 mchana hadi saa 1:00 usiku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)
(Hoja liliamuliwa na Kuafikiwa)*

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Wote wameafiki.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester hebu tulia.

Waheshimiwa Wabunge, tuna msiba na msiba huu; ninasikitika kuwatangazia kifo cha mtumishi mwenzetu Ndugu Rajabu Ramadhani Kipillah - Msaidizi wa Kumbukumbu Mwandamizi ambaye amefariki dunia tarehe 3 Februari, 2022 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma alikopelekwa kwa ajili ya kupata matibabu. Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma. Ofisi inaendelea kuwasiliana na familia ya marehemu kuhusu utaratibu wa mazishi. *Innalilah Wainailaih Rajiuun.*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa 8.00 mchana.

*(Saa 4:50 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu,
Tarehe 7 Februari, 2022 Saa Nane Mchana)*